JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI
SHULE YA SEKONDARI MUFUMBU
S.L.P 1032, SINGIDA

Namba za simu
Mkuu wa Shule 0787388792 / 0756378808
Makamu Mkuu wa Shule 0714962935/0757617199

Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi .........................................
S.L.P ..........................................................................

..........................................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA.........SHULE YA SEKONDARI MUFUMBU ILIYOPO HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA MK0A WA SINGIDA MWAKA………**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha….. katika shule hii mwaka…………, tahasusi ya ......................Shule ya Sekondari Mufumbu ipo Singida mjini kilometa Saba kusini mwa mji wa Singida kutoka stendi kuu ya mabasi "Misuna Bus terminal.Usafiri kutoka stendi hadi shuleni ni wa Bajaji / pikipiki. Nauli ni shilingi 1,000/= kwa bajaji ambapo unapandia kituo kinaitwa **Kona ya Mwakasege** mita (200) kutoka lango la stendi kuu upande wa magharibi, barabara ya Dodoma na Tsh4,000/= kwa pikipiki. Kwa wanaotokea barabara ya Dodoma shuka kituo cha Kisaki shule ipo kushoto mwa barabara. **Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni baada ya Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kutangaza tarehe ya kuanza kwa muhula wa masomo.**

***Karibu sana Mufumbu Sekondari.***

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Shule hii ni ya bweni na ni ya **wavulana pekee** kwa Tahasusi (combinations) za HGK na HGE: mahitaji ya shule ni kama ifuatavyo:

A. **Sare ya shule**

i. Shati mbili nyeupe za **tetroni** mikono mirefu ambazo hazibani mwili.
ii. Suruali mbili za rangi "Dark blue" zenye marinda mawili ya cross pembeni, mfuko mmoja wa nyuma usiokuwa na zipu wala kifuniko na upana chini ya miguu uwe inchi 17.
iii. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba navyenye visigino vifupi.
iv. Soksi jozi mbili nyeusi zisizo na mapambo wala maandishi.
v. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali wenye bakoni ya kawaida
vi. Begi la madaftari lisiwe la mfumo wa simu.
vii. Tai rangi ya Dark Blue yenye mistari ya pundamilia.

**Shamba Dress.**

i. Aje na T-shirt rangi ya dark blue aina ya "form six" isiyokuwa na maandishi yeyote;
ii. Suruari rangi ya Kijivu yenye marinda mawili ya cross pembeni mfuko mmoja wa nyuma usiokuwa na zipu wala kifuniko na upana chini ya miguu uwe inchi 17. ***Aje nazo akiwa amevaa.***

**Sare ya michezo**

i. Aje na jezi ya michezo rangi ya Blue (Taifa Stars)
ii. Viatu vya michew (raba).
iii. Aje na track suit ya rangi ya Kijivu mistari myeupe.

**NB. Track suti siyo sehem.u ya nguo za michezo**

**Angalizo**: Mwanafunzi haruhusiwi kufika shuleni na nguo nyingine yeyote tofauti na hizo alizoagizwa kwenye barua ya maelekezo.

B. **Michango muhimu ya shule**

Mchango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi kwa kila Mwanafunzi ni:

| | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5000/= |
| 3. | Nembo ya shule | 5000/= |
| 4. | Kitambulisho cha shule | 5000/=. |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango hii ilipiwe kupitia benki ya NMB kwenye akaunti namba **50801100176 MUFUMBU SECONDARY SCHOOL. Mwanafunzi aje na bank pay in slip ya michango hiyo (kumbuka kuandika majina kwenye BPS).**

**NB1**: Hakikisha mwanao ana kadi hai ya Bima ya Afya, ***shule haina gharama za matibabu kwa wanafunzi, hilo*** **ni *jukumu la* mzazi** na kwa ambao hawana Bima aje na Tsh 50,400/= kwa ajili ya Bima. (fedha ya Bima pamoja T- shirt zitalipwa shuleni wakati wa kuripoti, fedha hizo zisiwekwe kwenye akaunti ya shule}.

**NB2**: Mwanao anapoharibu mali ya shule atatakiwa kulipa gharama za utengenezaji.

**NB3**: Tunapendekeza mzazi kutupatia namba ya simu yenye whatsap kwa ajili ya taarifa muhimu za maendeleo ya mwanao na ya shule.

c) **Mahitaji ya Taalum.a**

i. Ream MBILI ( A4}, ya karatasi kwa mwaka
ii. Scientific calculator - function 991.
iii. Jalada au failijipya (spring file).
iv. Madaftari counter book quire4 nane kwa masomo ya msingi na quirel mawili kwa ajili ya mazoezi.
v. Saa kwa ajili ya kutunza muda.
vi. Unashauriwa kuja na vitabu vinavyoendana na Tahasasi (combination) ya mwanafunzi.

d) **MAHITAJI YA VIFAA VYA USAFI**

HGK -
i. Jembe lenye mpini.
ii. Ufagio wa 1 wa sakafu (soft broom).
iii. Squeezer moja.
iv. Ufagio wa chelewa.

HGE -
i. Fyekeo moja lenye mpini.
ii. Hard broom moja.
iii. Panga moja.
iv. Ufagio wa chelewa.

e) **MAHITAJI YA MALAZI NA CHAKULA**

i. Godoro (1) lenye inchi mbili na nusu mapana na urefu tatu kwa sita (21/2x 3 x 6).
ii. Shuka mbili (2) rangi ya light blue na foronya ya rangi ya ligh blue.
iii. Chandarua kimoja (1), pembe nne.
iv. Blanket moja.
v. Ndoo mbili (2) ndogo zenye mifuniko na galoni ya kutunzia maji ya kunywa kwa michepuo yote.
vi. Vyombo vya chakula kijiko, kikombe, bakuli na sahani.

**Angalizo**: *Mafuta ya kubadilisha rangi ya ngozi, mafuta yenye harufu kali (perfume, body spray)* ***HAZIRUHUSIWI***

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi , kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kunyoa nywele kwa mtindo usiokubalika na kufuga ndevu. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wawapo shuleni,huduma ya kunyoa inapatikana shuleni.
vii. Ulevi au unywaji pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
x. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xii. Kumiliki kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiii. Kudharau Bendera ya Taifa.
xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xv. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.
xvi. Kushiriki matendo ya uhalifu, uchochezi wa kisiasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xvii. Kumiliki simu

MUHIMU;

- Kosa la kumiliki simu/kutumia simu shuleni Mwanao atafukuzwa shule mara moja. Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa k:ulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- Ni marufuku kwa mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali. Pia kutumia na kukaa na dawa bila idhini ya daktari

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa mkuu wa shule. (Msiba au Ugonjwa)

4. **VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**
   a) Fornu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga wa hospitali ya Serikali)
   b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
   c) Fomu ya rnzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
   d) Picha(Passport size) nne (4). Mbili za Wazazi/Walezi yaani rnoja moja na mbili za Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za s1mu.
   e) Nakala moja ya cheti cha kuzaliwa
   f) Hati ya matokeo ya kidato cha nne (Result slip) halisi na nakala 1

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Mwanafunzi atasajiliwa tu baada ya kutekeleza maagizo haya na kukabidhi fomu zilizojazwa kikamilifu na si vinginevyo.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

AMAN! S. BANIGA
MKUU WA SHULE

KUU WA SHULL
MUFIBIJ SEKONDARI
SL.P.1032-SINGIDA

KIAMBATANISHO A.

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MUFUMBU

A: SEHEMU YA MWANAFUNZI
MWANAFUNZI AJAZE SEHEMU HII

1. Mimi............................................ninakubali kujiunga na Shule ya Mufumbu Sekondari katika Kidato cha.......... kwa machaguo ya(combination) .................
2. Mimi Mwanafunzi wa Mufumbu Sekondari, ninakubali kwamba:
   i. Nitafika Shuleni siku ya kufungua na bila kuchelewa kila muhula
   ii. Nitatii sheria zote za shule pamoja na kutoshiriki katika ulevi, migomo na migogoro ya aina yeyote.
   iii. Sitaleta shuleni wala kuvaa mavazi yasiyo ya heshima k.m. nguo za kubana, kofia, miwani ya giza, pete za urembo.
   iv. Nitatumia juhudi na maarifa yote kujiimarisha kitaaluma ikiwa ni pamoja na kuhudhuria vipindi na kufanya mazoezi na mitihani yote (k.v. usafi na elimu ya kujitegemea).

Saini ya Mwanafunzi ...................................... Tarehe ................................

B: SEHEMU YA MZAZI / MLEZI
MZAZI /MLEZI AJAZE SEHEMU HII

1. Mimi ........................................................nimekubali mtoto wangu ....................................................ajiunge na Shule ya Sekondari Mufumbu kuanzia tarehe ....................................

   Ninaahidi kwamba:
   i. Nitashirikiana na walimu kumlea mwanangu kitaaluma na kitabia. Nitamuonya na kumsisitiza mwanangu kutii sheria zote za shule na kuishi maisha mazuri kwa maadili ya kiuanafunzi.
   ii. Nitamkataza kuvaa nguo zisizo za heshima kama nguo za kubana, kofia, miwani ya giza n.k.
   iii. Nitampatia mtoto wangu nauli ya kuja shuleni na kurudi likizo bila kuchelewa.
   iv. Nitahakikisha anakuja shuleni siku ya kufungua kila muhula bila kuchelewa.

2. Anwani yangu ya kudumu ________________________________

   Sahihi ya Mzazi / Mlezi__________________ Tarehe________________ (Tafadhali njoo na fomu hii unapokuja shuleni ikiwa imejazwa).

# *OFISI YA WAZIRI MKUU TAMISEMI*
## SHULE YA SEKONDARI MUFUMBU

FOMU YA MAELEZO BAYANA (PERSONAL PARTICULARS) KWA AJILI YA USAJILI
IJAZWE NA MZAZI / MLEZI

1. Jina kamili la mwanafunzi kama alivyojiandikisha kwenye mtihani wa Kidato cha Nne..............................................
2. Jina kamili la Baba / Mlezi ............................(a) Anwani ya Baba / Mlezi ....................................... (ii) Namba ya simu ya Baba / Mlezi kazini.......................... Nyumbani -.............................. (iii) Mtaa/ Kijiji .......................................... Kata ..........................Tarafa...................... Wilaya ........................ anakokaa.
3. Jina la Mama / Mlezi ..........................................................
(i) Anwani ya Mama / Mlezi -.................................................. (ii) Namba ya simu ya Mama / Mlezi ...................................................... Nyumbani.............................. (iii) Mtaa / Kijiji ...........................................Kata..................................Tarafa................................ Wilaya ............................................................ anakokaa.
4. Tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi ...........................................................
5. Mahali alipozaliwa.........................................Mkoa ...................................Wilaya.............................. Kijiji/ Mtaa...............................................................
6. Kazi ya Baba / Mlezi.......................................................................................................
7. Kazi ya Mama / Mlezi .....................................................................................................
8. Je mwanafunzi anacho kilema chochote? ..............Kijaze..........................................
9. Taja ndugu watatu ambao wanaweza kutoa msaada kwa mwanao

| NA. | JINA | KAZI | UHUSIANO | NA. YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |

TAREHE.....................................SAHIHIYA MZAZI/MLEZI.........................

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A:**

TO: The Medical Officer From:....................................
---------------------------------------------- ..........................................
....................................................... .......................................

Student's full name..................................

Please examine the above named as to his/ her physical and mental fitness for a full - time Advanced Level of Secondary Education studies. The examination should include the following ineligible in case of a defect.

I. (a) Eyesight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Limbs
(e) Venereal Diseases
(f) Leprosy
(g) Epilepsy
(h) Neuroses
(i) Other serious diseases

Date: ................. Signature..."""

HUF MBIJ SEKUNDARI
SL.P.I032-SINGIDA

**PARTB:**

**MEDICAL CERTIFICATE"**
**(To be completed by a Government Officer)**

I have examined the above - named and consider that he / she is physically fit / unfit and mentally fit / unfit for a full – time Advanced Level of Secondary Education studies.

I. (a) Eyesight (b)Hearing
(c) Speech d) Limbs
(e) Vuneral I Diseases (f)Leprosy
II. Neuroses :..... .. " ..................
Other serious disease ..
III. Date: Name & Signature: Station:
Designation:

**VITABU VYA MASOMO MBALIMBALI**

SOMO LA GEOGRAPHY

1. Principles of physical geography by FJ monk house
2. Uninterested regional study on human and economic geography by D.T. Msabila
3. Essentials of Practical Geography by Josephat Mwita
4. Physical geography in diagram by Bunnett.
5. Statistical methods and the geographers by s. Gregory

MASOMO MENGINE

1. Aje na vitabu vya somo la Historia, English language na Economics vinavyotumika kwa kidato cha tano na sita.

**NB 1:** Mwanafunzi anatakiwa kuchagua kitabu kimojawapo au vyote kati ya namba mbili (2) na nne (4)

**NB 2: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekua wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHARI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI /MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA KUWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOORODHESHWA HAPO JUU YA FOMU.**